# Wakulima waomba wafugaji wazuiwe

RAIA MWEMA, 10/5/2022 Pg 15

Na Ibrahim Yassin, Songwe

WANANCHI jamii ya wakulima wilayani hapa, wameiomba Serikali kuzuia wafugaji kuingiza mifugo na kulisha mazao yao shambani katika bonde la Iseche, hali iliyotishia mapigano na hata mauaji.

Asilimia 90 ya wananchi hapa ni wakulima ambao hutegemea kuendesha maisha yao kulima mazao ya msimu wa mvua na kiangazi, lakini mwaka huu huenda wasivune kutokana na kundi la wafugaji kuingiza na kulisha mifugo kwenye mashamba yao.

Vincent Emmanuel wa bonde la Iseche, alisema mifugo mingi katika bonde hilo lenye rutuba, inatoka maeneo ambayo awali walikubaliana wawe wanaingiza kila Agosti mara wavunapo mazao, lakini kwa msimu huu, wameingiza hata kabla ya kuvuna, hivyo mifugo hiyo inakula mazao hali iliyozua taharuki.

Bidius Talimba mkulima wa Iseche, alisema kwa msimu huu bado hawajaanza kuvuna, lakini tayari ekari kadhaa zimeliwa na ng'ombe kwa makusudi, ambapo wafugaji wanaingiza mifugo nyakati za jioni wakati wakulima wameondoka na wasipodhibitiwa na wao wanaweza kufanya uamuzi mgumu na wa hatari.

Gaudence Otto, mkulima na Mwenyekiti wa Kijiji cha Iseche, alisema eneo hilo ni la wakulima, hao wafugaji wanatoka maeneo ya milimani kufuata malisho, lakini wao hawakuwafukuza, badala yake waliweka utaratibu kwa maandishi, kuwa kuanzia Novemba msimu wa kilimo mifugo yote ipelekwe maeneo ya milimani, ambako hakuna mashamba, na waingize mifugo Agosti wakati wamevuna, lakini wamekaidi makubaliano hayo.

Nawal Patani, Diwani wa Mwambani, alisema hilo la wakulima na wafugaji alilipeleka kwenye kikao cha Baraza la Madiwani ikaamuliwa mifugo iondolewe maeneo hayo na wao wasubiri utekelezaji na hayuko tayari kuona umwagaji damu unatokea kwenye kata yake.

Alisema bonde la Iseche lina ekari zaidi ya 2,000 za mazao ya mpunga, mahindi, mtama, ufuta, alizeti na mbogamboga ambazo zinalisha wilaya nzima na hata nje ya wilaya, wafugaji wasipodhibitiwa, kunaweza kutokea baa la njaa na hata mapigano ya wakulima na wafugaji, kwani wakulima hawatakubali wapoteze nguvu kazi zao.

"Mkuu wa Wilaya aliendesha operesheni ya kuondoa mifugo mashambani na kupiga marufuku uingizaji mifugo, lakini wafugaji ndiyo kwanza wameongeza kasi ya kuingiza hali inayowatia hofu ya kukosa chakula mwaka huu," alisema Patani.

Mwenyekiti Sambila alisema suala la wakulima kuingiza mifugo kwenye mashamba ambayo hayajavunjwa halikubaliki, hivyo alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri akae na watendaji wake kitengo cha mifugo, waone namna na kudhibiti hilo.

Mbunge wa Songwe, Philipo Mulugo aliagiza madiwani wa jimbo hilo kuhamasisha wananchi, kuwa mwaka huu mazao yamegoma hivyo kichache watakachopata wasikiuze chote, na pia wakawaeleze wananchi kulima mazao ya muda mfupi, ili kuzuia baa la njaa linaloweza kujitokeza.



. Ashantu Kijaji, akizungumza na baadhi ya wakurugenzi wa mashirika
: baada ya Bajeti ya Wizara yake kupitishwa bungeni jana. (Picha na Deus

Scanned with CamScanner

mawasiliano lafanyika

# Wavuvi kupatiwa vifaa vya kisasa

**Na MWANDISHI WETU,** *Uvinza*

SERIKALI imesema kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo watawapatia vifaa vya kisasa vya kuvulia wavuvi wanaoishi kandokando ya ukanda wa Ziwa Tanganyika na maeneo mengine ili viwasaidie kuongeza thamani ya zao la dagaa.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema vifaa hivyo vitasaidia kupunguza upotevu wa kitoweo hicho, baada ya kuvuliwa.

Ulega aliyasema hayo juzi wakati wa ziara yake aliyoifanya katika vijiji vya Buhingu na Katumbi vilivyopo wilayani Uvinza, mkoani Kigoma.

Alibainisha kuwa Rais Samia Suluhu Hassan, amedhamiria kukuza uchumi wa buluu katika kutengeneza miundombinu mizuri ya kuchakata dagaa na mazao mengine ya samaki ili kuwaongezea thamani na kuwawezesha wavuvi kuuza kwa bei nzuri na wananchi wanufaike na zao hilo.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, tunaendelea kutengeneza miundombinu mizuri ya kuchakata dagaa na mazao mengine ya samaki katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao na kuyaongezea thamani ili yauzwe kwa bei nzuri ndani na nje ya nchi."

"Tunataka tuone zao la dagaa ambalo huku Kigoma linazalishwa kwa wingi linainua maisha ya watu, hatutaki kuona hata dagaa mmoja anapotea kwa kuharibika au kuoza. Lengo letu ni kuona ukanda wote huu wa Ziwa Tanganyika mnanufaika ipasavyo kupitia dagaa," alisema

Alisema wanawapatia wavuvi hao vifaa

UHURU
MEI 10, 2022
P.5 K

> **Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, tunaendelea kutengeneza miundombinu mizuri ya kuchakata dagaa na mazao mengine ya samaki...**
>
> Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega

vikiwemo boti, injini, nyavu, kamba na taa, lengo likiwa ni kufanya uvuvi endelevu na kulifanya zao la dagaa kuwa la kimkakati ili liwe chachu ya maendeleo kwa wavuvi hapa nchini.

Aliwataka wananchi wanaoishi kandokando ya ukanda wa Ziwa Tanganyika kuendelea kutunza na kuhifadhi mazalia ya samaki ili uvuvi katika eneo hilo uwe endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Hanaf Msabaha, alisema kuna haja serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kuanzisha miradi ya ufugaji wa samaki wilayani humo, ili samaki wapatikane muda wote.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mradi wa Tuungane ambao unatekelezwa mkoani Kigoma, Lukindo Hiza, alisema tayari wameshirikiana na uongozi wa wilaya kujenga bwalo la kisasa litakaosaidia kupunguza upotevu wa dagaa na kuogeza thamani ili wauze kwa bei nzuri zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Scanned with CamScanner

UHURU ME 10, 2022
Pg 6.



NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Mradi wa Tuungane, Lukindo [illegible] (wa tatu kulia) kabla ya kukabidhi vifaa vya [illegible] dagaa kwa wavuvi wa kijiji cha [illegible], wilayani Uvinza, mkoani Kigoma, jana. (Na Mpiga picha wetu).

Scanned with CamScanner

# Wazalishaji kuku walia bei sokoni

NIPASHE MEI 10/2 Pg 7.

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa kiwanda cha Animal Care kilichoko Mlandizi Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Dk. Salaa Hamdun ameiomba serikali kusaidia kudhibiti bei ya kuku sokoni ili wafugaji wapate faida katika biashara hiyo.

Dk. Salaa alitoa ombi hilo jana baada ya Mwenge wa Uhuru kupita katika kiwanda chake na kukagua shughuli za uzalishaji zinazofanyika.

Alisema bei ya kuku sokoni bado ni ndogo ambayo inambana mkulima kwa kushindwa kupata faida ukilinganisha gharama za vyakula vya kuku hali ambayo wakati mwingine inasababisha baadhi yao kushindwa kuendelea na biashara.

"Serikali yetu ingeweza kutusaidia kwa wafugaji wetu, kusimamia masoko yao na kudhibiti bei mfano wanaouza kuku na maziwa bado bei ni ndogo ukilinganisha na gharama za vitu vingine kutokana na hali hiyo hata sisi tunaathirika moja kwa moja," alisema.

Alisema kwasasa wanakabiliana na kikwazo cha malighafi hususani zile wanazotoa nje ya nchi kama soya wanazotoa Zambia na Malawi, lakini wakati mwingine mahindi hasa pale yanaporuhusiwa kwenda nje inaawaathiri wawekezaji wa viwanda vya ndani.

Dk. Salaa alisema katika kiwanda hicho wanatengeneza fursa za moja kwa moja kwa wafugaji ambao wako katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Kiwanda hicho ambacho kinazalisha vyakula vya mifugo na virutubisho kinatumia malighafi za mahindi, dagaa na alizeti kimejikita pia katika kutoa elimu ya ufugaji kwa vijana.

Mkurugenzi huyo alisema kwa sasa wameweza kutoa ajira za moja kwa moja 200 na kwamba kitendo cha Mwenge wa Uhuru kufika katika kiwanda hicho wanaimani itazidi kufungua fursa mbalimbali.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Sahil Geraruma, amepongeza uwekezaji wa kiwanda hicho ambao unakwenda kupunguza tatizo la ajira.

Scanned with CamScanner

# Dagaa kuwa zao la kimkakati Kigoma

NIPASHE MEI 10, 2022 PG 8

**Na Mbaraka Kambona,** UVINZA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wanatengeneza miundombinu mizuri na kuwapatia wavuvi wanaoishi kandokando ya ukanda wa Ziwa Tanganyika na maeneo mengine vifaa vya kisasa vya uvuvi ili viwasaidie kuongeza thamani ya zao la dagaa na kupunguza upotevu wa zao hilo baada ya kuvua.

Ulega aliyasema hayo wakati wa ziara yake aliyoifanya katika vijiji vya Buhingu na Katumbi vilivyoko wilayani Uvinza mkoani Kigoma Mei 6 - 7, 2022.

Akizungumza na wavuvi wa vijiji hivyo kwa nyakati tofauti alisema Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kukuza uchumi wa buluu na ndio maana inatengeneza miundombinu mizuri ya kuchakata dagaa na mazao mengine ya samaki ili kuyaongezea thamani na yaweze kuuzika kwa bei nzuri na wananchi wafaidike na zao hilo.

"Tunataka tuone zao la dagaa ambalo huku Kigoma linazalishwa kwa wingi linainua maisha ya watu, hatutaki kuona hata dagaa mmoja anapotea kwa kuharibika au kuoza, lengo letu ni kuona ukanda wote huu wa Ziwa Tanganyika mnanufaika ipasavyo kupitia dagaa," alisema.

Aliongeza kuwa wanawapatia wavuvi hao vifaa ikiwamo boti, injini, nyavu, kamba na taa lengo likiwa ni kufanya uvuvi endelevu na kulifanya zao la dagaa kuwa la kimkakati ili liwe chachu ya maendeleo kwa wavuvi hapa nchini.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo tunaendelea kutengeneza miundombinu mizuri ya kuchakata dagaa na mazao mengine ya samaki katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao hayo na kuyaongezea thamani ili yauzwe kwa bei nzuri ndani na nje ya nchi," alifafanua.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Hanafi Msabaha, alisema kuwa kuna haja serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kuanzisha miradi ya ufugaji wa samaki wilayani humo ili samaki waweze kupatikana muda wote.

Mkurugenzi wa Mradi wa Tuungane ambao unatekelezwa mkoani Kigoma, Lukindo Hiza alisema tayari wameshirikiana na uongozi wa Wilaya ya Uvinza kwa ajili ya kujenga mwalo wa kisasa utakaosaidia kupunguza upotevu wa dagaa na watawezakuwaongezea thamani ili wawauze kwa bei nzuri zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

in HIV Aids and TB with a national responsibility to research on human diseases, as well facilitating other

NIMR in conducting research at the hospital to control TB in the country, he added.

GUARDIAN MAY 10, 2022, Pg 2.

# Govt, development partners improving infrastructure for Kigoma fishermen

DAHTN

**By Guardian Reporter, Uvinza**

THE government in collaboration with development partners is creating good infrastructure for fishing and provides fishermen along Lake Tanganyika shores with modern fishing gear to add value to their sardines (dagaa) and reduce losses after fishing.

The remarks were made by the Livestock and Fisheries Deputy Minister Abdallah Ulega during his inspection visit to Buhingu and Katumbi villages in Uvinza District, Kigoma Region at the weekend.

Speaking at different times to the residents of the two villages, Ulega said President Samia Suluhu Hassan vows to strengthen the blue economy and that is why the government is creating good infrastructures for processing sardines and other fish products to add value to their products.

"We like to see Kigoma Region produce large quantities of sardines to raise the standard of living of its residents, we do not like to see even a single sardine is lost or go bad, our aim is to see the entire Lake Tanganyika zone benefit through sardines," he said.

He added that they provide fishing equipment including boats, outboard motors, fishnets and ropes to make sardines fishing a strategic activity for the development of the fishermen.

He called on residents living along the western shores of the Lake to continue taking care of fish breeding grounds to make the occupation sustainable for the present and future generations.

For his part, Uvinza District Commissioner, Hanaf Msabaha said there was need for the government to work together with development partners to establish fish farming projects in the district.

The Director of Tuungane Project being implemented in Kigoma Region, Lukindo Hiza said already they have been collaborating with Uvinza District officials for the construction of a modern fishing port that will help reducing after harvest losses of the sardines.

> **We like to see Kigoma Region produce large quantities of sardines to raise the standard of living of its residents, we do not like to see even a single sardine is lost or go bad, our aim is to see the entire Lake Tanganyika zone benefit through sardines**

Scanned with CamScanner